# TARGETER WINGS

## JUNIOR SECONDARY SCHOOL ASSESSMENT

## GREDI YA SABA - 2024

Wings 001

**Muda: Saa 1 dakika 20**

# KISWAHILI

**Jina** ______________________________

**Shule** ______________________________

**Nambari ya Usajili:** ____________________ **Tarehe** ____________________

**Instructions:**

*(a) Andika jina lako, la shule, nambari ya usajili na tarehe kwenye vihasho uliopewa.*

*(b) Jibu maswali yote kwenye karatasi hili.*

| MTAHINI PEKEE | | | |
|---|---|---|---|
| Swali | Upeo wa alama | Alama ya mwanafunzi | Kiwango cha utendaji |
| 1-30 | Alama 50 | | |
| Jumla | 50 | | |



CamScanner

***Swali 1 hadi 4***

**UFAHAMU WA KUSOMA**

Zamani, wanyama wa porini walikuwa na mashamba yao na walilima, wakapanda na kuvuna kwa ushirikiano. Hata hivyo Sungura alijitenga nao. Aliweza kuwadanganya wenzake na wakamsaidia kulima shamba lake la njugu karanga lakini yeye alihepa kuwasaidia katika mashamba yao.

Wanyama walipogundua ujanja wake, walikataa kumsaidia. Sungura hakujua sababu ya kutosaidiwa. Alipowauliza, walimwambia kuwa yeye hasaidii yeyote hivyo basi hakustahili kusaidiwa. Sungura akafahamu wazi kuwa upweke ni uvundo na akaanza kuwafuata kwa siri mnyama mmoja baada ya mwingine kuomba usaidizi. Wote wakakataa kumsaidia. Mnyama wa mwisho kufuatwa na Sungura alikuwa Mbuzi. Wanyama wote walifikiri kuwa maadamu Mbuzi ana ila ya upumbavu na ulafi angedanyika haraka.

Sungura akamwambia mbuzi, "ukinipandia njugu zangu mwaka huu, tutagawa sawasawa tutakachovuna."

Mbuzi akamwamini Sungura na kumjibu, "Nimekubali kukupandia karanga, lakini nataka makubaliano yetu kuwa ya siri. Usimwambie mnyama mwingine."

Baada ya kuwaza kidogo, Sungura alisema, "shamba hili ni kubwa sana. Peke yako, hutaweza kulilima na kulipanda lote. Nenda ukawaambie shamba hili sasa ni lako na umelinunua kutoka kwangu". Mbuzi alifanya hivyo na wanyama wakamsaidia kulima.

Chui aligundua kuwa wamedanganywa siku ya pili walipomwona Sungura akipanda njugu. Kwa hasira, walimketisha Sungura na kumwamuru awaeleze ukweli. Ukweli ulipobainika, walimlaumu mbuzi na akaamrishwa kumlipa kila mnyama aliyefanya kazi.

1. Unadhani ni kwa nini Sungura alikataa kushirikiana na wenzake? (alama 2)

_______________________________________________

2. Kwa nini wanyama walikataa kumsaidia Sungura kulima shamba lake? (alama 1)

_______________________________________________

3. Wanyama waliamini kuwa mbuzi angedanywa. (alama 1)

_______________________________________________

4. Adhabu ya Mbuzi kwa kuwadanganya wanyama ilikuwa ni gani? (alama 2)

_______________________________________________

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali 5 hadi la 8.***

Kwa kweli mavazi huweza kumpamba mwanadamu au kumwaibisha. Mavazi humfanya mtu kuwa mtanashati au mrembo anapotaka na vilevile humuaibisha pia anapotaka.

Lengo kuu hasa la watu kuvaa mavazi ni kujisitiri japo zipo sababu tele kama vile kuhifadhi utamaduni wa mtu, kujikinga na baridi, kuvutia machoni pa watu na kutaka kutambuliwa kwa cheo.

Jambo la kushangaza ni kuona kuwa ile sababu kuu ya kuvaa mavazi siku hizi imetupiliwa mbali na wanadamu hasa vijana. Mavazi mafupi mafupi ya kubana mwili yamekuwa ni mitindo wala si aibu kwa wengi. Nguo nyingine huonyesha maumbile ya mwili namna yalivyo. Mavazi sampuli hii ndiyo yanayotia fora kwa vijana wetu. Jamani! Ulimwengu umebadilika upesi hivi kwamba vijana hawa kutoka mbele ya wazazi wao au jamaa zao bila kukatazwa au kuonywa. Jamani, hawajui kuwa mwacha mila ni mtumwa?

Wamaasai wanasifika ulimwenguni kote kwa kuhifadhi na kudumisha utamaduni wao hasa katika mavazi. Mchango wa teknolojia katika uigaji wa tamaduni za kigeni ni mkubwa mno. Vijana wetu wanapaswa kuchuja wanayoona mtandaoni ili wasiige kila waonalo. Wazazi nao wawe mstari wa mbele kukemea uigaji usiofaa. Kumbuka, ukicha mwana kulia mwisho utalia wewe.

5. Watu huvaa mavazi kwa sababu nyingi. Sababu kuu ni ipi? ____________ (alama 1)

6. Mavazi yana uwezo gani kwa mwanadamu? ____________ (alama 2)



CamScanner

7. Vijana wanalaumiwa kwa sababu gani? (alama 2)
   A. Kufuata tamaduni za kigeni.
   B. Kutembea bila nguo.
   C. Kuvaa mavazi yasiyofaa na kuiga tamaduni za kigeni.
   D. Kuacha mila zao na kuvaa mavazi ya kujisitiri.
8. Wamaasai wanasifika ulimwenguni kutokana na jambo gani? (alama 2)
   A. Kulinda kabila lao.
   B. Kuhifadhi na kudumisha utamaduni wao.
   C. Kuvaa mavazi yanayowabana.
   D. Kuchuja wanayotazama mtandaoni.

***Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali 9 hadi 12.***

Jinsia ni hali ya kuwa mtu wa kike au kiume. Kinyume na hapo zamani. Jinsia zote ni muhimu. Watoto wanapozaliwa tunaamini kuwa wao ni kipawa cha thamani kutoka kwa Mungu. Awe ni mtoto wa kike au wa kiume wote ni sawa. Hatuna budi kuwapenda na kuwatunza kwa moyo wa dhati. Wao ni tunu isiyoweza kulinganishwa na kitu chochote duniani.

Watoto wa kike au wa kiume ni tumaini letu la baadaye. Wao ni viongozi wa siku za usoni. Kwa hivyo wanapaswa kuhifadhiwa na kuandaliwa vizuri ili waweze kukabiliana na majukumu haya mazito yanayowangoja. Watoto wanapaswa kutimiziwa mahitaji yao ya kimsingi bila mapendeleo kama vile kupewa elimu ya msingi isiyo na malipo, huduma bora za afya na kupewa chakula cha kutosha chenye lishe bora.

Jinsia zote zinaposhirikishwa katika maamuzi hasa yanayowahusu na kuheshimu mawazo yao, kujihisi kuwa wao pia ni muhimu katika jamii. Usibague jinsia ya kike au ya kiume kwa kuficha habari wanazopaswa kujua. Ukifanya hivyo utakosea kwani nao pia wana haki ya kufahamishwa yanayoendelea katika mandhari yao.

9. Unadhani ni jambo gani lililo tofauti kuhusu jinsia wakati wa zamani na sasa? (alama 2)

   ______________________________________________

10. Kwa nini watoto wanastahili kupendwa na kutunzwa kwa moyo wa dhati? (alama 3)

   ______________________________________________

   ______________________________________________

11. Mbali na mahitaji ya kimsingi ya mtoto ambayo yametajwa katika kifungu hiki, taja hitaji jingine la kimsingi la mtoto. ______________________________ (alama 1)
12. Maana ya neno mandhari kama lilivyotumiwa ni ______________________________ (alama 1)

**SARUFI**

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 13 hadi 17. Kwa kila nafasi, umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

__13__ ni hali ya kutenda haki kila wakati bila ya kupendelea upande __14__. Ni mwenendo __15__. Mtu __16__ haya yote huitwa mwadilifu. Mtu ambaye ni mwadilifu hupendwa na __17__ sana na takribani kila mtu.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 13. | Uaminifu | Upendo | Umoja | Uadilifu |
| 14. | yeyote | yoyote | wowote | kokote |
| 15. | mwema | chema | kwema | pema |
| 16. | mzingatifu | anayezingatia | asiyezingatia | anayechangaza |
| 17. | kudhaminiwa | kutamaniwa | kuthaminiwa | kudaminiwa |

18. Chagua neno lililo tofauti na mengine kwenye kadi hii. (alama 1)

| |
|---|
| **Kiswahili** |
| **Kisumu** |
| **Alhamisi** |
| **Maziwa** |

______________________________________________



CamScanner

19. Kisawe cha neno ugonjwa ni maradhi au ndwele. Je, kisawe cha maskini ni ______________________ (alama 1)

20. Yafuatayo ni majina ya ndege wa porini.
*(i) Kanga*
*(ii) Kasuku*
*(iii) Mwewe*
*(iv) Chiriku*
*(v) tai*
Majina haya hufuatana vipi kwenye kamusi? (alama 3)

______________________________________________________________________

21. ***Andika jibu la maagano:*** Buriani ______________________________________(alama 2)

22. ***Jaza nafasi kwa kuchagua jibu sahihi:***
______________________ aliniazima kitabu chake cha hadithi. **(Wao, Yeye, Wewe, Nyinyi).** (alama 1)

23. ***Chagua kwa kupigia mstari kiwakilishi kiashiria katika sentensi:***
Hawa walinisaidia sana nilipowahitaji nyumbani kwangu. (alama 2)

24. ***Akifisha sentensi ifuatayo:***
Miti ina manufaa mengi hutupa matunda, hurembesha mazingira na kusafisha hewa. (alama 3)

______________________________________________________________________

25. Tunga sentensi ukitumia neno **Mheshimiwa** (alama 2)

______________________________________________________________________

26. ***Andika wingi wa:***
Maasi yake yalisababisha afungwe gerezani. (alama 2)

______________________________________________________________________

27. ***Jaza nafasi kwa kutumia kiambishi sahihi:***
_______ takapofanyiwa mkutano pamepangwa na wanafunzi. (alama 1)

28. Sentensi: Charo na Mwanjuma wanasoma insha walizoandika ni katika kauli ya kutenda. Iandike upya katika kauli ya kutendeana. (alama 3)

______________________________________________________________________

29. ***Kinyume cha neno kifupi ni kirefu. Andika sentensi ifuatayo kwa kutumia kinyume cha neno lililopigiwa mstari.***
Zainabu ni msichana <u>mwema</u>. (alama 2)

30. ***Tunga sentensi ukitumia maneno yafuatayo:*** (alama 2)
thamini / dhamini

______________________________________________________________________



CamScanner

# TARGETER WINGS

## JUNIOR SECONDARY SCHOOL ASSESSMENT

# GREDI YA SABA - 2024

Wings 001

## SEHEMU B:

## KISWAHILI : INSHA

***MUDA: Dakika 40***

**Jina** ______________________________________________

**Shule** ______________________________________________

**Nambari ya Usajili:** ____________________ **Tarehe** ____________________

**SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI**

1. Kwenye nafasi zilizoachwa hapo juu **andika jina lako na jina la shule yako.**

2. Sasa fungua karatasi hii, soma kichwa cha insha kwa makini na uandike insha yako kwenye nafasi uliyoachiwa.

**Kijitabu hiki kina kurasa 4 zilizopigwa chapa.**

*© Hutungwa na kuchapishwa na Targeter Educational Publishers Ltd. Email:info@targeterpublishers.co.ke*

**FUNGUA KURASA**

CamScanner

**Andika insha ya kusisimua kuhusu sherehe uliyohudhuria**